**MUHTASARI WA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 07/12/2020 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

1. Mhe. Kashinje Machibya - Usagara - Mwenyekiti – Mwenyekiti wa Halmashauri
2. Mhe. Rahma E. Fidel - Bulemeji - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Dome K. Manyasa - Busongo - Mjumbe
4. Mhe. Ezekiel Kanzaga - Kijima - Mjumbe
5. Mhe. Faustine Mchenya - Nhundulu - Mjumbe
6. Mhe. Daniel Makoye - Kanyelele -Mjumbe
7. Mhe. Ngagizi M. Zozozo - Lubili -Mjumbe
8. Mhe. Ruth R. Seni - Kijima - Mjumbe
9. Mhe. Amina A. Mwandu - Mbarika -Mjumbe
10. Mhe. Angela G. Isandiko - Usagara - Mjumbe
11. Mhe. Muganyizi Leonard Feruzi- Misungwi - Mjumbe
12. Mhe. Mathew M. Makoye - Ukiriguru - Mjumbe
13. Mhe. Fidel Lazaro - Kasololo - Mjumbe
14. Mhe. Bilarmini Hilary - Koromije - Mjumbe
15. Mhe. Enos Mihayo - Gulumungu - Mjumbe
16. Mhe. Beatrix Kabulule - Usagara -Mjumbe
17. Mhe. Marco L. Kadala - Buhingo - Mjumbe
18. Mhe. Ng'wanza M. Nyahehe - Mwaniko - Mjumbe
19. Mhe. Raphael A. Kaboya - Isenengeja - Mjumbe
20. Mhe. Jojo Mohamed - Ilujamate - Mjumbe
21. Mhe. Luzambya L. Simuda - Buhunda - Mjumbe
22. Mhe. Daniel Masasi Busalu - Misasi - Mjumbe
23. Mhe. Joel J. Dogani - Mbarika - Mjumbe
24. Mhe. Malale P. Lutonja - Mabuki - Mjumbe
25. Mhe. Dotto Lugwisha - Misasi - Mjumbe
26. Mhe. Christina L. Nyandu - Mamaye - Mjumbe
27. Mhe. Bernard D. Polycarp - Igokelo - Mjumbe
28. Mhe. Mayila S. Maguha - Shilalo - Mjumbe
29. Mhe. Paul M. Kishinda - Fella - Mjumbe
30. Mhe. Adelina Mathias - Buhunda - Mjumbe
31. Mhe. Samson N. Mbizo - Mondo - Mjumbe
32. Mhe. Hindu Y. Kimila - Misungwi - Mjumbe
33. Mhe. Yona M. Shimbewangoso- Mamaye - Mjumbe
34. Mhe. Jogoli K. Mayombo - Sumbugu - Mjumbe
35. Mhe. Edward Dawson - Idetemya - Mjumbe
36. Mhe. Monica N. Lushiku - Lubili - Mjumbe

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA.**

1. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti - Mbunge

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA**

1. Ndg. Kisena Mabuba - Katibu - Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Ndg. Leokadia G. Humera - Afisa Utumishi (W)
3. Ndg. Mwanajumbe Zuberi - Kaimu Afisa Mipango (W)
4. Ndg. Juliana Luhasile - Afisa Uvuvi (W)
5. Ndg. Willihelmina Nkunga - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
6. Ndg. Thomas Lutego - Afisa Habari (W)
7. Ndg. Dorcas P. Nigha - Afisa Nyuki (W)
8. Ndg. Mariam M. Simon - Kaimu Afisa Mazingira (W)
9. Ndg. Faustine Salala - Mthibiti Ubora (W)
10. Ndg. Cresencia Mwalongo - Afisa Tarafa Mbarika
11. Ndg. Sindagulu Jonas - Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani
12. Ndg. Benjamini Sarakikya - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
13. Ndg. Renatus Nyasebwa - Kny.Afisa Ardhi na Maliasili (W)
14. Ndg. Mwanjia Hassani - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika (W)
15. Dr. Zabron Masatu - Mganga Mkuu (W)
16. Ndg. Josephat Yamo - Kny. Afisa Manunuzi (W)
17. Ndg. Perpetua Chonja - Afisa Tarafa Usagara
18. Ndg. Henry Rumanyika - Kaimu Mwanasheria (W)
19. Ndg. Christina Katole - Afisa Manunuzi (W)
20. Ndg. Peter K. Michael - Afisa Tarafa – Misungwi
21. Ndg. Bernadetha Sanga - Mratibu wa UKIMWI
22. Ndg. Gloria Buname - Mratibu TASAF (W)
23. Ndg. Dismas S. Dotto - Afisa Afya (W)
24. Ndg. Yusuph Lubuga - Afisa Usafirishaji (W)
25. Ndg. Manyanza J. Mageme - Katibu TSC
26. Ndg. Gloria Kaywanga - Afisa Tarafa Inonelwa
27. Ndg. Faustine Savel - Kaimu Mweka Hazina (W)

29.Ndg. Dickson Kawovela - Kaimu Afisa Uchaguzi (W)

30.Ndg. Diana Kuboja - Afisa Elimu Sekondari (W)

**WATENDAJI WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

Hakuna

**WAGENI WAALIKWA**

1. Ndg.Sweda Juma - Mkuu wa Wilaya
2. Ndg.Deo Madete - DSO
3. Ndg.Gambadu Samwel - Mwenyekiti CCM
4. Ndg.Latifa B. Malimi - Katibu CCM
5. Captain EL Mateni - MJA (W)
6. Ndg.Mbaribu E. Lyimo - DIA
7. Eng. C. Masasila - DM
8. Eng. Bujiku W.M - Meneja MWAUWASA
9. FC Rajabu Mohamed - ZIMAMOTO
10. Ndg.Masumbuko Daniel - Mwandishi wa Habari TBC

11. Ndg.John F. Bendera - TANESCO & REA
12. Ndg.Gervas Mbaya - Mwandishi BMG TV
13. Ndg.Antony Chuwa - Mwandishi COK TV
14. Ndg.Twalib Salum - Mwandishi Gazeti Mwananchi

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Gelda Kweyamba
2. Ndg. Martha S. Mbise

**AGENDA.**

(1) Kufungua mkutano.
(2) Kuapisha Madiwani
(3) Madiwani kutoa tamko
(4) Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Halmashauri na Makamu Mwenyekiti
(5) Kuunda kamati za kudumu za Halmashauri
(6) Madiwani kuwasilisha anuani za kudumu
(7) Kupitisha ratiba ya vikao vya kisheria kwa kipindi cha Julai 2020 – Julai 2021
(8) Kupokea taarifa toka kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
(9) Kufunga mkutano.

**MUHT NA. 01/12/2020: KUFUNGUA MKUTANO.**

Katibu kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti ili azindue Baraza aliwakaribisha wageni wote katika jengo jipya la Halmashuri na kumshukuru Mungu kwa kuwakutanisha tena kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Halmashauri baada ya Baraza kuvunjwa mwezi Mei 2020.

Alieleza kuwa katika jengo jipya kuna ukumbi mkubwa na mzuri kwa ajili ya mikutano hivyo aliwakaribisha wote kuutumia. Alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue mkutano.

Mwenyekiti aliwakaribisha wageni wote na kuwapongeza Madiwani kwa kuaminiwa na wanachi na kuwachagua na wananchi.

Alieleza utaratibu wakuendesha mkutano wa kwanza wa Baraza kwamba mkutano utafanyika kwa kufuata sheria, taratibu na miongozo iliyowekwa kisheria.

Aidha kamati zote za kudumu zitachaguliwa na matokeo yatatangazwa kwa uwazi kuzingatia Demokrasia. Alifungua mkutano saa 6:03 mchana.

**MUHT. NA. 02/12/2020: KUAPISHA MADIWANI.**

Mwanasheria alieleza taratibu na umuhimu wa kiapo kwa Madiwani kwamba yeyote ambaye hatakula kiapo kwa sababu yeyote ile hataruhusiwa kuanza kutekeleza majukumu yake.

Baada ya maelezo hayo alimkaribisha Hakimu Mkazi kwa ajili ya kuwaapisha Madiwani.

Madiwani wote 36 waliapa mmoja mmoja na kusaini fomu ya kiapo.

**MUHT. NA. 3/12/2020: MADIWANI KUTOA TAMKO.**

Kamishna wa Sekretarieti ya Madiwani kwa viongozi wa Umma alieleza kuwa mtu yeyote akipata nafasi ya Uongozi wa Umma anatakiwa atoe tamko la rasilimali na maadili ndani ya siku 30.

Alieleza kuwa tamko lina umuhimu kwani husaidia viongozi kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za kudumu, pia huongeza imani kwa wananchi. Baada ya maelezo hayo aliwaongoza Wahe. Madiwani walisimama na kutoa ahadi ya Uadilifu kwa viongozi wa Umma.

Aidha baada ya Wahe. Madiwani kutoa ahadi hiyo Katibu aliwatambulisha viongozi na wageni katika mkutano huo ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Wageni kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoani Mwanza, Afisa Usalama wa Wilaya, TARURA, TANESCO, MWAUWASA, TANESCO, REA ambao walitoa pongeza kwa Wahe. Madiwani kuchaguliwa kuwatumikia wananchi, walisisitiza kufanya kazi pamoja ili kujenga na kuongeza maendeleo ya Wilaya na nchi kwa ujumla.

**MUHT. NA. 4/12/2020: UCHAGUZI WA MWENYEKITI NA MAKAMU MWENYEKITI WA HALMASHAURI.**

Katibu alieleza kuwa tayari walipokea majina ya Wagombea nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri kutoka chama cha siasa chenye Madiwani Misungwi kwenye Halmashauri na kwa mujibu wa mwongozo wa kuendesha mkutano wa kwanza wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Wilaya ndiye atakateongoza na kusimamia uchaguzi huo. Katibu alisoma majina ya wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kama ifuatavyo:-

**(A)Nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri wagombea ni:-**

(i) Mhe. Kashinje Machibya Erasto – CCM

**(B)Nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri**

(i) Mhe Rahma Emmanuel Fidel - CCM

Katibu Tawala (W) aliwapa nafasi wagombea kuomba kura kwa wajumbe ambapo alieleza kuwa kwa kuwa kila nafasi ina mgombea mmoja tu basi zitapigwa kura za NDIYO na HAPANA. Wajumbe walipewa karatasi za kupigia kura mmoja baada ya mwingine na kupiga kura kwa faragha ambapo matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

**A. Nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri**

(i) Wajumbe waliopiga kura ni 36

(ii) Kura zilizoharibika ni 0

(iii) Kura za ndiyo ni 36

Hivyo Katibu Tawala (W) alimtangaza Mhe. KASHINJE MACHIBYA ERASTO kuwa ndiye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

**B. Nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri**

(i) Wajumbe waliopiga kura ni 36

(ii) Kura zilizoharibika ni 0

(iii) Kura za ndiyo ni 36

Hivyo Katibu Tawala (W) alimtangaza Mhe. RAHMA EMMANUEL FIDEL kuwa ndiye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

Baada ya uchaguzi Katibu Tawala (W) aliwapongeza viongozi walioshinda na kuwashukuru viongozi wa chama cha Mapinduzi kwa ushirikiano mkubwa kipindi cha uchaguzi pia alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa kuiongoza Halmashauri kwa kipindi chote ambacho Wahe. Madiwani hawakuwepo.

Aliwahimiza Wahe. Madiwani kwenda kutekeleza shughuli za maendeleo na kutatua kero za wananchi kwa maendeleo ya Kata, Wilaya, Mkoa na Nchi kwa ujumla

**MUHT. NA. 5/12/2020: KUUNDA KAMATI ZA KUDUMU.**

Mwenyekiti aliwashukuru Wahe. Madiwani kwa kumchagua na wao kuchaguliwa katika Kata zao pia alikipongeza chama cha Mapinduzi kwa ushindi huo.

Aliunda kamati za kudumu kama ifuatavyo:-

**KAMATI YA HUDUMA ZA KIJAMII**

1. Mhe.Enos Mihayo Nestory
2. Mhe.Kashinje Machibya
3. Mhe.Marco Lucas Kadala
4. Mhe.Kanzaga K. Ezekiel
5. Mhe.Mathew Makoye
6. Mhe.Raphael A Kaboya
7. Mhe.Ng'wanza M. Nyahehe
8. Mhe.Jojo Mohamed
9. Mhe.Ngagizi Zozozo
10. Mhe.Hindu Y. Kimila
11. Mhe.Beatrice K. Kipanda
12. Mhe.Monica N. Lushiku
13. Mhe.Edward R.Dawson
14. Mhe.Faustini Msafiri
15. Mhe. Daniel Makoye

Wajumbe walimchagua Mwenyekiti wa kamati Mhe. Enos Mihayo kwa kura za NDIYO.

**2) KAMATI YA UCHUMI.**

1. Mhe.Joel Japhet Dogani
2. Mhe.Kashinje Machibya
3. Mhe.Bernard D. Polycarp
4. Mhe.Bilarmini Hilary
5. Mhe.Ruth Seni
6. Mhe.Amina Mwandu
7. Mhe. Dome K. Manyasa
8. Mhe.Yona Shimbewangoso
9. Mhe.Malale P. Lutonja

10. Mhe.Fidel Kabidi
11. Mhe.Jogoli K. Mayombo
12. Mhe.Daniel Busalu
13. Mhe.Luzambya Luhweja
14. Mhe.Samson N.Mbizo
15. Mhe.Dotto Lugwisha

Wajumbe walimchagua Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe Joel Japhet Dogani kwa kura za NDIYO.

**3) KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO**

1. Mhe. Kashinje Machibya Erasto - Mwenyekiti wa kamati.
2. Mhe. Alexander Mnyeti(Mb)
3. Mhe. Rahma E. Fidelis
4. Mhe. Angella Gabriel
5. Mhe. Adelina M. Malale
6. Mhe. Christina Nyanda
7. Mhe. Muganyizi Feruz
8. Mhe. Mayila S. Maguha
9. Mhe. Paulo Kashinde
10. Mhe. Joel Japhet Dogan
11. Mhe. Enos Mihayo

**4. KAMATI YA MAADILI YA MADIWANI.**

1. Mhe.Bilarmini Hilary
2. Mhe.Muganyizi Feruz
3. Mhe.Lucy Seni
4. Mhe.Hindu Yahya

Wajumbe walimchagua Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe Bilarmini Hilary kwa kura za NDIYO.

**KAMATI YA UDHIBITI UKIMWI**

1. Mhe. Rahma Fidelis - Mwenyekiti wa kamati.
2. Mhe.Daniel Makoye
3. Mhe.Jogori Mayombo
4. Mhe.Monica Nungule
5. Mhe.Beatrice Kabulule

**6. WAJUMBE ALAT MKOA**

1. Mhe. Dotto Lugwisha
2. Mhe.Daniel Busalu

**7. BODI YA AJIRA**

1. Mhe. Mayila Maguha

**MUHT. NA. 6/12/2020: MADIWANI KUWASILISHA ANUANI ZA KUDUMU**

Katibu alitoa maelezo kwa Wahe. Madiwani kwamba wanatakiwa kuwasilisha anuani zao za kudumu ili kurahisisha mawasiliano, Wahe. Madiwani waliwasilisha anuani zao za kudumu katika fomu maalum.

**MUHT. NA. 7/12/2020: MAPENDEKEZO YA RATIBA YA VIKAO VYA KISHERIA KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 HADI JUNI 2021**

Katibu aliwasilisha mapendekezo ya ratiba ya vikao kwa kipindi cha mwezi Julai 2020, hadi mwezi Juni 2021 ambapo wajumbe walipitia na kupitisha mapendekezo ya ratiba hiyo.

**MUHT. NA. 8/12/2020: KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI (W).**

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Halmashauri ya Misungwi kuanzia mwezi Mei 2020 hadi Novemba 2020 kama ifuatavyo;

**i) MAPATO YA NDANI.**

Aliwasilisha taarifa ya mapato ya ndani kwamba kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ilikuwa imekusanya kiasi cha Tshs. 2,341,506,157.02/= sawa na asilimia 101.8 ya makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ambayo ni Tshs. 2,300,000,000/=.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imepanga kukusanya kiasi cha Tshs. 2,300,000,000/= ambapo kuanzia mwezi Julai hadi Novemba 2020 ilikusanya Tshs. 948,281,238.4 kutoka mapato ya ndani sawa na asilimia 41.23 ya fedha pangwa kwa mwaka.

**ii) UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.**

Aidha aliwasilisha taarifa ya fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa ndani ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuanzia mwezi Mei hadi 30 Juni, 2020 kiasi cha Tshs. 1,290,795,579.96 na kutumika kiasi cha Tshs. 681,833,766.83 sawa na asilimia 58.82 ya fedha tolewa.

Pia aliwasilisha taarifa ya fedha zilizopokelewa nje ya mpango wa bajeti kiasi cha Tshs. 1,323,272,245.92 na kutumika kiasi cha Tshs. 298,957,981.93 sawa na asilimia 22.59 ya fedha zilizotolewa.

**iii) IDARA YA MIPANGO**

Alieleza kuwa Halmashauri ilianzisha Kampuni ambapo ndani ya Kampuni kuna Miradi 03 ambayo ni Duka la Dawa muhumu lililopo Hospitali ya Wilaya na Kiwanda cha Maziwa kilichopo Mabuki. Aidha katika makabidhiano ya mali ya Halmashauri na Kampuni, Mali zilizohamishiwa kwenye Kampuni ni Mashine 01 ya kufyatulia Tofali,

Makoleo 04, Tolori 01 la kubebea tofali,Vibao 369, Mifuko ya Saruji 100 na kiasi cha Tshs.24,547,983.00 imeingizwa kwenye akaunti ya Kampuni.

**iv) IDARA YA AFYA**

Aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya Wilaya Misungwi iliendelea kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya afya kwa kusogeza huduma karibu na wananchi. Ikiwa pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kupitia fedha toka Serikali Kuu Tshs. 500,000,000/= unaendelea na majengo mawili yameanza kujengwa ambayo ni Maabara na Jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na ujenzi wake upo hatua za ukamilishaji.

**v) IDARA YA ELIMU.**

Aidha Halmashauri iliendelea kusimamia na kufuatilia utoaji wa huduma ya Elimu ikiwa ni pamoja na utoaji wa Elimu bila malipo kwa shule 140 za Msingi na shule 27 za Sekondari, kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo toka fedha za EP4R kwa shule 05 za msingi na shule 02 za Sekondari kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 14, vyoo matundu 25 ambapo ujenzi unaendelea.

**vi) UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.**

Katibu alieleza kuwa Halmashauri imekuwa ikitenga 10% toka mapato ya ndani (4% Wanawake, 4% Vijana 2% Walemavu), kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ilipanga kutoa kiasi cha Tshs. 200,964,000/= kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Walemavu, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 jumla ya fedha Tshs. 123,056,500/= zilitolewa kwa vikundi (vikundi vya wanawake 09, vijana 06 na walemavu 05)

Aidha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilipanga kutoa kiasi cha Tshs. 158,644,000/= hadi kufikia Novemba 2020 imetoa kiasi cha Tshs. 65,454,000/= kwa vikundi 10 vya wanawake, 02 vijana na 01 walemavu.

**vii) IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA**

Aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya wilaya Misungwi ilisimamia masuala ya kiutumishi ikiwemo kuwabadilisha miundo watumishi 101, katika Idara ya Afya 25, Utawala 4, Maendeleo ya Jamii 17, Mifugo na Uvuvi 1, Tehama 1, Mipango na Uchumi 5, Idara ya Ujenzi 1, Mazingira 1, Ugavi 1, Elimu Msingi 35 na Elimu Sekondari 9.

**viii) IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA.**

Aidha aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ilisimamia shughuli mbalimbali za kilimo, umwagiliaji na ushirika:-

1) Uvunaji na ununuzi wa zao la Pamba ambapo jumla ya tani 599.8 za Pamba zenye thamani ya Tshs. 516,213,000 zilinunuliwa.
2) Usambazaji wa mbegu za Pamba aina ya UKM 08 tani 117.345 za mbegu zimesambazwa katika AMCOS 40 zilizopo wilayani kwa ajili ya kuwagawia wakulima wa Pamba katika kata zote.

**ix) IDARA YA MIFUGO NA UVUVI.**

Ilielezwa kwamba Halmashauri ya wilaya inaendelea kufanya shughuli za mifugo na uvuvi ikiwa ni pamoja na:-

1) Zoezi la utoaji wa chanjo ya mifugo, ambapo jumla ya Ng'ombe 51,033 walichanjwa kati ya ng'ombe 84,700 sawa na asilimia 60, kuzuia ugonjwa wa chambavu na kimeta, kuku 2637 walichanjwa kukinga ugonjwa wa kideli.
2) Ilifanyika doria 03 za majini na kukamata zana za uvuvi haramu 76 zikiwemo kumbakumba 03, lubaluba 02, kokolo 01, nyavu za makila 70 chini ya inchi 6, na samaki wachanga waliokamatwa ni Kg. 35.

### x) KITENGO CHA NYUKI.

Aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ilifanikiwa kuhamasisha ufugaji wa Nyuki katika vikundi 22 kutoka vijiji vya Ilalambogo, Nyamayinza, Mwagimagi, Ngudama, Mwalogwabagole, Bukumbi, Iteja, Misungwi, Ndinga, Usagara, Isenengeja, kijima, Kasololo na Kijima, uvunaji wa jumla ya Kg 510 za asali zimevunwa kwa wafugaji Nyuki binafsi na vikundi kutoka katika vijiji vya Iteja, Misungwi, Usagara, Isenengeja na Kijima.

### xi) KITENGO CHA TEHAMA.

Halmashauri ya Wilaya ilitekeleza shughuli mbalimbali za kitengo ikiwa ni pamoja na kukamilisha ufungaji wa Mfumo wa kuimarisha ulinzi (CCTV CAMERA) katika jengo la Hospitali ya wilaya Misungwi ambapo camera 13 za ulinzi zilifungwa, kuweka mfumo mpya (Mobile Application) ya LGRCIS toleo la 4 katika POS 60 za kukusanya mapato ya Halmashauri

### xii)KITENGO CHA UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU.

Halmashauri Aidha katika utekelezaji wa shughuli za Idara ya Mazingira Halmashauri iliendelea kufanya uhakiki na ufuatiliaji wa tathimini ya adhari kwa mazingira (EIA) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji safi na usafi wa mazingira Shilalo, Mahando, Lubili, Ibinza, Mabale – Misasi.

Pia ilifanya ukaguzi wa mazingira katika shughuli za uchenjuaji wa madini ya dhahabu Shilao, Nyambiti, Buhunda, Isenengeja na Mbalama.

### xiii) KITENGO CHA SHERIA.

Aliwasilisha shughuli za kitengo cha sheria kwamba Halmashauri iliendelea kusimamia mashauri mbalimbali ambapo kuna jumla ya kesi 25 kati ya hizo kesi 10 ni za madai, 05 za migogoro ya kikazi na kesi 10 za migogoro ya ardhi. Aidha kati ya kesi zote 25 kesi 02 ambazo ni migogoro ya kikazi zimeisha na kesi 07 zipo katika hatua ya makubaliano na kesi 16 zipo katika hatua mbalimbali.

### (xiii) KITENGO CHA UCHAGUZI

Katika shughuli za kitengo cha Uchaguzi alieleza kuwa Halmashauri ilisimamia uchaguzi kwa mwaka 2020 ambao ulihusisha uchaguzi wa Madiwani, Mbunge na Rais ambapo kwa Jimbola Misungwi Madiwani katika Kata 27 na Mbunge kupitia chama cha Mapinduzi walipita bila kupingwa na kufanya kuwa na ushindi wa asilimia 100, na

upande wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia tiketi ya chama cha Mapinduzi tulipata ushindi wa asilimia 98.7

**(xiv) IDARA YA ARDHI NA MALIASILI**

Halmashauri iliendelea na shughuli za Idara ya Ardhi na Maliasili ikiwa ni pamoja na :-

(i) Uandaaji wa hati ambapo jumla ya hati 123 ziliandaliwa.

(ii) Upimaji wa viwanja na ramani ambapo jumla ya viwanja 2,479 vilipimwa.

(iii) Upandaji wa miti ambapo miche ya miti 17,000 ilipandwa kwa wadau mbalimbali vijijini.

**(xv) KITENGO CHA MANUNUZI**

Halmashauri iliendelea kufanya manunuzi katika Idara mbalimbali yenye thamani ya Tshs. 650,530,883.16 kwa ajili ya ununuzi wa vitu mbalimbali vikiwemo vifaa vya ofisi, vifaa vya TEHAMA na vifaa kwa ajili ya chanjo.

Taarifa ilipokelewa.

**MUHT. NA. 09/12/2020: KUFUNGA MKUTANO.**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge mkutano kwa kuwa agenda zote zilikuwa zimejadiliwa, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki katika mkutano wa baraza la kwanza la Madiwani na kabla ya kufunga mkutano aliwakaribisha wageni waliokuwa wamealikwa ili waongee.

**(I) MKUU WA WILAYA YA MISUNGWI.**

Mkuu wa Wilaya ya Misungwi aliwapongeza Wahe. Madiwani kwa kuchaguliwa na alisisitiza mambo yafuatayo;

(i) Kila mmoja ajitume kuwatumikia wananchi na kuibeba Ilani ya Chama ambayo ina lengo la kuboresha maendeleo ya Taifa.

(ii) Kufanya kazi kwa bidii kwani wananchi wana imani kubwa na chama cha Mapinduzi, viongozi pamoja na Rais wao Dr. John P. Magufuli.

(iii) Ushirikiano na wananchi uwe mkubwa kwa kuwasikiliza, kuwashauri na kutatua kero zao ili kuinua maendeleo ya Wilaya.

(iv) Kipindi cha 2020-2025 ni kipindi ambacho kinategemewa kuwa na utekelezaji mkubwa hivyo kila mmoja akasimamie maendeleo ya Kata yake ikiwa ni pamoja na kujenga miundo mbinu ya Shule, usimamizi wa miradi na mapato ya Kata.

(iv) Wananchi wahamasishwe katika shughuli za kilimo kwa kuwa mvua zinaendelea kunyesha.

**(II) KATIBU WA CCM**

Katibu wa Chama cha Mapinduzi alisema kuwa uchaguzi umeisha hivyo ushirikiano wa wataalamu na Wahe. Madiwani uwe mkubwa kwani hao ndio wanategemewa ili kutekeleza ilani ya uchaguzi wa mwaka 2020-2025.

Aliwashukuru wajumbe kwa kuchagua viongozi wa Halmashauri pamoja na Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

**(II) MWENYEKITI WA CCM.**

Mwenyekiti wa Chama alimpongeza Mwenyekiti na Makamu mwenyekiti wa Halmashauri kwa kuchaguliwa ambapo alisema Wahe. Madiwani wana kazi kubwa ya kusimamia maendeleo na ahadi zote zilizoaidiwa kwa wananchi kwenye ilani ya uchaguzi 2020 – 2025.

Mwenyekiti kabla ya kufunga kikao alisema yafuatayo:-

(i) Kazi ya kutambua miradi na kuitekeleza ni jukumu la wote kwani Ilani ya uchaguzi ya 2020-2025 inamatatamanio makubwa ya kuboresha maendeleo ya Umma.

(ii) Halmashauri ya Misungwi inatakiwa kuendelea kupata Hati safi hivyo kama wawakilishi wa wananchi inapaswa kuwa na ushirikiano katika usimamizi wa shughuli zote za maendeleo pamoja na mapato ya Halmashauri. Alifunga kikao saa 11:18 jioni.

**UMETHIBITISHWA**

……………………………………… ………………………………
**KATIBU** **MWENYEKITI**

**TAREHE** 31/03/2021 **TAREHE** 31/03/2021.